# SEHEMU YA PILI: TUNAADHIMISHA

## TUNAMWADHIMISHA MUNGU, NAFSI ZAKE NA KAZI ZAKE

***120. Tumuadhimishe nani?***
- Tumuadhimishe Mungu pekee siku zote za maisha yetu kwa tumaini la kumuadhimisha milele. "Ee Mungu wangu, Mfalme, nitakutukuza, nitalihimidi jina lako milele na milele. Kila siku nitakuhimidi, nitalisifu jina lako milele na milele" *(Zab 145:1-2).* "Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una yeye milele. Amina" *(Rom 11:36).*

***121. Je, tumuadhimishe Mungu katika Nafsi zake tatu pia?***
- Ndiyo, tumuadhimishe Mungu katika Nafsi zake tatu pia: Baba kama asili ya umungu na ya uhai wote, Mwana kama Neno wake aliyejifanya mtu atukomboe, tena Roho Mtakatifu kama Upendo wao ambao unawaunganisha na kututakasa. Pamoja na viumbe vyote tuwaimbie usiku na mchana, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja!" *(Ufu 4:8).* "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" *(Yoh 4:24).*

***122. Tumuadhimishe Mungu kwa jinsi alivyo au kwa maajabu anayotutendea?***
- Tumuadhimishe Mungu kwa jinsi alivyo, halafu kwa maajabu anayotutendea tangu awali, ambayo anatujulisha kidogo jinsi alivyo. "Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele" *(Zab 136:1).*

***123. Tumuadhimishe Mungu hasa kwa maajabu gani?***
- Tumuadhimishe Mungu hasa kwa maajabu aliyoyatenda katika Yesu, lakini pia katika Maria na wengine ambao wamefanana naye na kutuonyesha uwezo wa neema yake kwetu. "Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo

ametuneemesha katika huyo Mpendwa" *(Ef 1:5-6).* Yeye atakuja "ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki" *(2Th 1:10).*

***124. Tumuadhimishe Mungu kwanza kwa njia gani?***
- Tumuadhimishe Mungu kwanza kwa kumsikiliza kwa makini na kumuitikia kwa imani. "Masikio ya watu wote yalikisikiliza kitabu cha torati... watu wote walilia, walipoyasikia maneno ya torati" *(Ne 8:3,9).* Kunyamaza ni sehemu ya ibada yoyote: tunahitaji kimya ili tuelewe tunachoambiwa na tunachosema. "Nisikieni nyote na kufahamu" *(Mk 7:14).* "Hamjui mnaloliomba" *(Mk 10:38).*

***125. Je, ibada zetu ziishie katika kusadiki?***
- Hapana, ibada zetu zisiishie katika kusadiki, kwa kuwa tangu Agano la Kale Mungu aliagiza matendo mbalimbali ya ibada yanayolisha imani. "Hili ndilo agano langu utakalolishika, kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako: Kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa... Mtoto wa siku nane atatahiriwa kwenu" *(Mwa 17:10,12).* "Mwanakondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka mmoja... Kusanyiko lote la mkutano wa Israeli watamchinja jioni... Ni Pasaka ya Bwana... Siku hii itakuwa ukumbusho kwenu, nanyi mtaifanya iwe sikukuu kwa Bwana" *(Kut 12:5,6,11,14).* Kwetu sisi Wakristo ni yale tuliyoagizwa na Yesu ili yatuletee wokovu. "Aaminiye na kubatizwa ataokoka" *(Mk 16:16).*

***126. Kanisa linaitaje ibada hizo tulizoagizwa na Yesu?***
- Kanisa linaita ibada hizo tulizoagizwa na Yesu sakramenti, yaani mafumbo. Ziko saba: Ubatizo, Kipaimara, Ekaristi, Kitubio, Mpako wa Wagonjwa, Daraja na Ndoa. Ndiyo "mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono" *(Eb 6:2)* tuliyoyapata kupitia Mitume. Tujihadhari na madhehebu yaliyopunguza sakramenti hizo saba tulizoachiwa na wema wa Yesu kwa kuwa alijua tunavyozihitaji.

***127. Je, tuishie katika kusadiki na kuadhimisha mafumbo?***
- Hapana, tusiishie katika kusadiki na kuadhimisha mafumbo, kwa kuwa imani na sakramenti zinadai kutekelezwa maishani. "Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?... Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana" *(Rom 6:2-3; 12:1).* "Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" *(Math 5:16).*

***128. Matendo yetu yasipomtukuza Mungu, maana yake nini?***
- Matendo yetu yasipomtukuza Mungu, maana yake mafumbo hayakuadhimishwa vizuri. "Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa" *(Yak 2:26).*

***129. Mungu ametuagiza matendo maalumu ya ibada kwa sababu gani?***

- Mungu ametuagiza matendo maalumu ya ibada kwa kuzingatia umbile letu, kwamba binadamu ni umoja wa roho na mwili, hivyo anahitaji mwili na hisi zake ili kuingiza chochote rohoni na kutokeza yaliyomo katika roho yake isiyoonekana. Ndiyo sababu Yesu alipoletewa kiziwi mwenye utasi "akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate, akamgusa ulimi, akatazama juu mbinguni, akaugua, akamwambia, 'Efatha', maana yake, 'Funguka!'" *(Mk 7:33-34).* Hizo zote ni ishara wazi kwa milango yetu ya fahamu.

***130. Je, hisi zetu zote zinaweza kutumika kuadhimishia mafumbo?***

- Ndiyo, hisi zetu zote zinaweza kutumika kuadhimishia mafumbo, kila moja kadiri ya uwezo wake: macho kwa kuona, pua kwa kunusa, kinywa kwa kuonja na kusema, mwili mzima kwa kugusa na kutenda, lakini hasa masikio kwa kupokea maneno yaletayo uzima wa Kimungu. "Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima" *(Yoh 6:63).* "Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia... Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo" *(Rom 10:13-14,17).*

***131. Kwa nini maneno ndiyo muhimu zaidi kuadhimishia mafumbo?***

- Maneno ndiyo muhimu zaidi kuadhimishia mafumbo kwa sababu yanafafanua ishara nyingine na kuzitia nguvu ya kututakasa. "Kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno" *(Ef 5:25-26).* Pasipo maneno hapana sakramenti yoyote.

***132. Ishara za mafumbo zimetokana na nini?***

- Ishara za mafumbo zimetokana na viumbe (maji, mafuta, mkate, divai n.k.) na maisha ya jamii (kuosha, kupaka, kula na kunywa pamoja n.k.) na historia ya wokovu (kunyunyiza na kuzamisha, kuwekea mikono, kula Pasaka, n.k.), lakini ni kwa kuagizwa na Yesu kwamba zinabeba kazi yake ya kuokoa na kutakasa. "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" *(Lk 22:19).*

***133. Maneno na ishara vinaweza kubadilishwa na nani?***

- Maneno na ishara vinaweza kubadilishwa na waandamizi wa Mitume, waliokabidhiwa na Yesu mamlaka ya kuendeleza kazi yake katika mazingira mbalimbali hata mwisho wa dunia. "Amin, nawaambieni: Yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni, na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni" *(Math 18:18).* Hao Maaskofu wanakiri hawawezi kamwe kuyabadilisha yale ambayo Yesu aliyaweka kuwa ya lazima kama yalivyo mafumbo yenyewe. "Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi" *(1Kor 11:23).* Mengine yote wanaweza kuyapanga na kuyarekebisha kadiri ya mazingira, kuanzia lugha, wakilenga daima wokovu wa watu.

***134. Faida ya kupanga taratibu za ibada ni ipi?***
- Faida ya kupanga taratibu za ibada ni hasa kuhakikisha yote yafuate usahihi wa imani na maadili, yakidumisha umoja na upendo, badala ya kumuachia kiongozi au mwingine yeyote aseme na kufanya anavyotaka. Mitume wenyewe walianza kazi hiyo, wakidhibiti hata karama. "Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga. Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu. Na manabii wanene wawili, au watatu, na wengine wapambanue. Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa neno, yule wa kwanza na anyamaze... Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana. Lakini mtu akiwa mjinga, na awe mjinga... Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu" *(1Kor 14:26-30,37-38,40).* Polepole taratibu ziliongezeka na ibada zikapata mtiririko rasmi wa kueleweka: ndizo liturujia za mashariki na za magharibi ambazo zinaweza kuwa mbalimbali mradi zisipishane upande wa imani.

***135. Mhusika mkuu wa mafumbo hayo ni nani?***
- Mhusika mkuu wa mafumbo hayo ni Mungu ambaye kwa njia hiyo anazidi kutufanyia maajabu alivyoyafanya Yesu alipokuwa duniani. Kama tunda la kutukomboa kwa kifo na ufufuko wake, Baba anatujaza humo Roho Mtakatifu kama advansi ya uzima wa milele. "Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi yake aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake" *(Ef 1:13-14).*

***136. Sisi tunahusika na mafumbo hayo kama nani?***
- Sisi tunahusika na mafumbo hayo kama walengwa ambao tuyatumie vema ili yazae matunda yote yaliyokusudiwa na Mungu. Ndiyo kiini cha ukuhani wetu ambao tunashiriki ule wa Kristo tangu tubatizwe. "Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo" *(1Pet 2:4-5).*

***137. Tunapoadhimisha mafumbo hayo, Mungu anatukuzwa vipi?***
- Tunapoadhimisha mafumbo hayo, Mungu anatukuzwa kwa kuwa ndivyo anavyotufanya "tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo... tupate kuwa sifa ya utukufu wake" *(Ef 1:4,12).* Tukipokea neema hiyo tunampatia ibada, sifa na shukrani na tunazidi kumuomba atujaze Roho Mtakatifu kwa njia ya Mwanae. "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele.

Amina” *(Ef 3:20-21).*

***138. Je, mafumbo yote saba yanazaa matunda yaleyale?***

- Hapana, mafumbo yote saba hayazai matunda yaleyale, bali Yesu aliweka kila moja kwa lengo maalumu, litupatie Roho Mtakatifu kadiri ya nafasi na haja fulani ya maisha yetu. Ubatizo, kipaimara na ekaristi vinatuingiza katika fumbo la Pasaka tuweze kuishi upya kama wana wa Mungu. Kitubio na mpako wa wagonjwa vinatuponya roho na hata mwili. Daraja na ndoa zinatufanya wahudumu wa Kanisa na wa familia. Ni muhimu tujue tunachohitaji na tukipate vipi. “Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili. Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. Lakini kama tungejipambanua nafsi zetu, tusingehukumiwa” *(1Kor 11:29-31).*

***139. Tushiriki mafumbo hayo mara ngapi?***

- Tushiriki mafumbo hayo kadiri ya umbile la kila mojawapo. Kuna “ubatizo mmoja” *(Ef 4:5)* kwa sababu ni kuzaliwa upya “kwa maji na kwa Roho” *(Yoh 3:5),* jambo lisiloweza kurudiwa. Vilevile katika kipaimara na daraja, karama inayopatikana kwa kuwekewa mikono na mwandamizi wa Mitume haifutiki, inadai kuchochewa tu. “Nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu” *(1Tim 1:6).* Kumbe tunahitaji ekaristi mara nyingi, kwa sababu ni chakula cha roho. “Bwana, sikuzote utupe chakula hiki” *(Yoh 6:34).* “Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo” *(1Kor 11:26).*

***140. Je, mafumbo yote yanaweza kuadhimishwa na yeyote?***

- Hapana, si mafumbo yote yanaweza kuadhimishwa na yeyote, bali mengine yanahitaji mhudumu wake awe amepewa daraja inayoshirikisha uwezo ambao Yesu aliwapa Mitume wake. “Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu. Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake; akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita Mitume” *(Lk 6:12-13).* “Yesu aliwaambia tena, ‘Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami nawapeleka ninyi’. Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, ‘Pokeeni Roho Mtakatifu’” *(Yoh 20:21-22).* Kwa kuwa Waprotestanti hawana sakramenti ya daraja, kati yao zinapatikana sakramenti zile mbili tu zisizohitaji padri, yaani ubatizo na ndoa.

***141. Je, tunapoadhimisha mafumbo hayo tuko peke yetu?***

- Hapana, tunapoadhimisha mafumbo hayo hatuko peke yetu, bali tunashiriki ibada ambayo Yesu anamtolea Baba milele. “Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao” *(Math 18:20).* Kwa kuungana na Kristo Kichwa, tunaungana na viungo vyote vya Mwili wake, vya duniani, toharani na mbinguni. “Ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa

mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkutano mkuu wa kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika, na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili" *(Eb 12:22-24).*

***142. Je, kuna nyakati za kufaa zaidi kumuadhimishia Mungu?***
- Ndiyo, kuna nyakati za kufaa zaidi kumuadhimishia Mungu. Yesu aliyesema, "Sikuja kutangua, bali kutimiliza" *(Math 5:17),* alifuata kalenda ya dini ya Kiyahudi, halafu kwa kufa na kufufuka amekuwa kiini cha ibada zetu zote. Hivyo Mitume waliadhimisha siku aliyofufuka kama "siku ya Bwana" *(Ufu 1:10)* ambapo wakutane "ili kumega mkate" *(Mdo 20:7)* wa ekaristi. Vilevile kwenye Pasaka hawakuadhimisha tu kazi ya Musa, bali ukumbusho wa Yesu. "Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo" *(1Kor 5:7).* Fumbo hilo ndio moyo wa mwaka wa liturujia, yaani wa mpangilio wa maadhimisho katika mzunguko wa mwaka. "Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo" *(Kol 2:16).*

***143. Je, kuna mahali pa lazima pa kumuadhimishia Mungu?***
- La! Hakuna mahali pa lazima pa kumuadhimishia Mungu, kwa kuwa yeye hafungwi na mahali. "Mungu je, atakaa kweli kweli juu ya nchi? Tazama, mbingu hazikutoshi, wala mbingu za mbingu; sembuse nyumba hii niliyoijenga!" *(1Fal 8:27).* "Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono" *(Mdo 17:24).* Hata hivyo sisi watu tunahitaji mahali maalumu kwa matendo yetu mbalimbali, na kumwekea Mungu mahali patakatifu. "Mwambieni mwenye nyumba, 'Mwalimu asema: Ki wapi chumba changu cha wageni, niile Pasaka humo, pamoja na wanafunzi wangu?' Naye mwenyewe atawaonyesha orofa kubwa, imeandikwa tayari; humo tuandalieni" *(Mk 14:14-15).*

***144. Hekalu ndiyo nini?***
- Hekalu ndipo tunapomuendea Mungu kwa ibada. Yesu aliheshimu na kutakasa hekalu pekee la taifa lake kama "nyumba ya Baba" yake *(Yoh 2:16),* lakini alitabiri kuwa litabomolewa moja kwa moja, na kuwa watu watapaswa kuabudu ndani yake aliye hekalu hai. "Wayahudi walisema, 'Hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita, nawe utalisimamisha katika siku tatu?' Lakini yeye alinena habari za hekalu la mwili wake" *(Yoh 2:20-21).* "Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho" *(Ef 2:22).* "Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi" *(1Kor 3:16-17).*

***145. Je, sanaa zinafaa kumuadhimishia Mungu?***
- Ndiyo, sanaa zinafaa kumuadhimishia Mungu kwa sababu tunapaswa kutumia kwa utukufu wake vipawa alivyotujalia, kama vile vya kujenga, kupamba, kuchonga, kuchora na kucheza. Kwa njia hizo tutokeze na kukoleza imani yetu na ya wenzetu. Mungu "amewajaza watu hao akili za moyoni, ili watumike katika kazi za kila aina, ya mwenye kuchora mawe, na kazi ya werevu, na ya mwenye kutia taraza, katika nyuzi za rangi ya samawi, na za rangi ya zambarau, na nyekundu, na kitani nzuri, na ya mwenye kufuma nguo; ya hao wafanyao kazi yoyote, na ya wenye kuvumbua kazi za werevu. Basi, Bezaleli na Oholiabu watatenda kazi, na kila mtu mwenye moyo wa hekima, ambaye Bwana amemtia akili na hekima ili ajue kufanya kazi hiyo yote kwa huo utumishi wa mahali patakatifu, kama hayo yote Bwana aliyoyaagiza" *(Kut 35:35-36:1).* "Maskani zako zapendeza kama nini, Ee Bwana wa majeshi!" *(Zab 84:1)*.

***146. Kati ya sanaa, muhimu zaidi ni ipi?***
- Kati ya sanaa, muhimu zaidi ni uimbaji, kwa kuwa unahusiana zaidi na Neno la Mungu, ukilitia maanani kwa uzuri wa muziki. Katika Agano la Kale, kitabu cha Zaburi ni nyimbo tupu za kutumia katika ibada. "Msifuni kwa mvumo wa baragumu; msifuni kwa kinanda na kinubi! Msifuni kwa matari na kucheza; msifuni kwa zeze na filimbi! Msifuni kwa matoazi yaliayo; msifuni kwa matoazi yavumayo sana!" *(Zab 150:3-5).* Agano Jipya pia linatuletea nyimbo nyingi. "Mjazwe Roho, mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu" *(Ef 5:18-19).* Mbinguni washindi wana "vinubi vya Mungu. Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwanakondoo" *(Ufu 15:2-3).*

***147. Kuimba ni kazi ya nani?***
- Kuimba ni kazi ya kusanyiko lote, yaani ya kila mwamini. Kwaya ziimbishe watu wamwadhimishe Mungu, zisiwaimbie tu na kuwanyima nafasi ya kuimba. "Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote, mtumikieni Bwana kwa furaha, njoni mbele zake kwa kuimba" *(Zab 100:1-2).* "Kila kiumbe kilichopo mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, 'Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwanakondoo, hata milele na milele'" *(Ufu 5:13).*

***148. Katika kutumia sanaa kwa ibada tuzingatie nini?***
- Katika kutumia sanaa kwa ibada tuzingatie utakatifu na ukweli, si uzuri tu. Zisiigeuze kamwe kuwa igizo wala tamasha, kwa kuwa lengo si kuchangamsha watu bali kumtukuza Mungu. Ziinue mioyo kwake, zitokeze na kuchangia maisha safi, zilete ujumbe sahihi kadiri ya imani na maadili, kama ilivyo lazima kwa mahubiri na mafundisho. "Watu hawa huniheshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu" *(Math 15:8-9).*

***149. Je, ni halali kuheshimu sanamu?***
- Ndiyo, ni halali kuheshimu sanamu kama viwakilishi vya Yesu, Mama yake na watakatifu wake, ambao zinaleta sura zao. Kwa msingi huo walimsihi Yesu "waguse hata pindo la vazi lake tu. Na wote waliogusa wakaponywa kabisa" *(Math 14:36).* "Mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote il msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo" *(Gal 6:14).*

***150. Wakati wa ibada tuvae vipi?***
- Wakati wa ibada tuvae namna inayodhihirisha malengo ya moyo wetu, hasa usafi na heshima, unyenyekevu na udugu. "Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki, kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote" *(Math 23:27).* "Akiingia katika sinagogi lenu mtu mwenye pete ya dhahabu na mavazi mazuri, kisha akiingia na maskini, mwenye mavazi mabovu; nanyi mkimstahi yule aliyevaa mavazi mazuri, na kumwambia, 'Keti wewe hapa mahali pazuri', na kumwambia yule maskini, 'Simama wewe pale', au 'Keti miguuni pangu', je, hamkufanya hitilafu mioyoni mwenu, mkawa waamuzi wenye mawazo mabovu?" *(Yak 2:2-4).* "Wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani, bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu" *(1Tim 2:9-10).* Kanisa si mahali pa mashindano: hatuendi kupendeza watu, ila Mungu. "Au mnalidharau kanisa la Mungu, na kuwatahayarisha hao wasio na kitu?" *(1Kor 11:22).*

## SAKRAMENTI ZA KUINGIZWA KATIKA UKRISTO

***151. Sakramenti ya kwanza daima ni ipi?***
- Sakramenti ya kwanza daima ni ubatizo, kwa kuwa ndio kupata uzima mpya kwa kushiriki kifo na ufufuko wa Yesu, inavyodokezwa wazi zaidi mtu akizamishwa na kutolewa majini. "Tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" *(Rom 6:4).* Sakramenti nyingine zote ama zinastawisha ama zinafufua uzima huo wa Kimungu ambao ni sharti la kuingia mbinguni. "Amin, Amin, nakuambia: Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu" *(Yoh 3:5).*

***152. Kwa nini ubatizo unafanyika kwa maji?***
- Ubatizo unafanyika kwa maji kwa kuwa ndiyo ishara ya usafi na ya uhai unaotupatia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. "Nami nitawanyunyizia maji

safi, nanyi mtakuwa safi; nitawatakaseni na uchafu wenu wote, na vinyago vyenu vyote. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu" *(Ez 36:26-27).* "Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwanakondoo" *(Ufu 22:1).*

***153. Ubatizo unatolewa pia kwa maji machache tangu lini?***
- Ubatizo unatolewa pia kwa maji machache tangu mwanzo. Kutokana na umuhimu wa sakramenti hiyo Yesu ametuagiza twende kubatiza watu duniani kote. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonyesha waamini walivyotekeleza agizo hilo katika mazingira mbalimbali, sio tu yalipopatikana maji mengi. Hivyo Paulo alipokuwa ndani ya nyumba "akasimama akabatizwa" *(Mdo 9:18).* Kumbe Yohane Mbatizaji hakusogea mbali na mto Yordani, akisubiri watu wamuendee kutoka maeneo yote ya nchi ile kame. "Alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele" *(Yoh 3:23).*

***154. Je, ubatizo uliotolewa na Yohane Mbatizaji ulikuwa sakramenti?***
- Hapana, ubatizo uliotolewa na Yohane Mbatizaji haukuwa sakramenti, kwa sababu yeye alikuwa mtangulizi tu wa Yesu, mwanzilishi wa sakramenti zote. "Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto" *(Math 3:11).* Paulo aliuliza watu, "'Mlibatizwa kwa ubatizo gani?' Wakasema, 'Kwa ubatizo wa Yohane'. Paulo akasema, 'Yohane alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu'. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu" *(Mdo 19:3-5).*

***155. Tofauti kubwa kati ya ubatizo wa Yohane na ule wa Yesu ni zipi?***
- Tofauti kubwa kati ya ubatizo wa Yohane na ule wa Yesu ni kwamba sakramenti inategemea imani kwa Kristo na kutushirikisha kifo na ufufuko wake. "Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo" *(Gal 3:27).* Ndivyo inavyoondolea dhambi zote na kuingiza katika uzima wa Utatu Mtakatifu. Kwa sababu hiyo Yesu aliagiza tubatize "kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" *(Math 28:19).* Maneno hayo ndiyo muhimu zaidi katika sakramenti hiyo. Maji peke yake, hasa yakiwa mengi, yanaweza kuosha mwili, lakini si roho. Kumbe ubatizo unaotuokoa "siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu" *(1Pet 3:21).*

***156. Je, watoto wachanga wanaweza kubatizwa?***
- Ndiyo, watoto wachanga wanaweza kubatizwa kwa sababu hawakatai neema ya Mungu. Wanafunzi wa Yesu walipotaka kuwazuia wasiletwe kwake "alichukizwa sana, akawaambia, 'Waacheni watoto wadogo waje

kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amin, nawaambieni: Yeyote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa" *(Mk 10:14-15).* Yeremia aliambiwa, "Kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa" *(Yer 1:5).* Yohane Mbatizaji alitabiriwa "atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye" *(Lk 1:15).*

***157. Mbona watoto wachanga hawawezi kuelewa kinachofanyika?***
- Ingawa watoto wachanga hawawezi kuelewa kinachofanyika, Mungu anaweza kuwamiminia rohoni mwanga wa imani. "Vinywani mwa watoto wachanga na wanyonyao umeiweka misingi ya nguvu" *(Zab 8:2).* "Elisabeti aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake... kwa shangwe" *(Lk 1:41,44).* "Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga. Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyopendeza mbele zako" *(Math 11:25-26).*

***158. Je, watu wazima wanaweza kuelewa sakramenti kwa dhati?***
- Hapana, watu wazima hawawezi kuelewa sakramenti kwa dhati, kwa kuwa zote ni mafumbo yanayotuzidi. Basi, kama Petro alipooshwa miguu, tumuachie Bwana atufanyie kazi anavyojua yeye. "Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye" *(Yoh 13:7).* Kisha kuoshwa tuzidi kuchimba mafumbo hayo kwa mwanga wa Neno na wa Roho Mtakatifu. "Je, mmeelewa na hayo niliyowatendea?... Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo" *(Yoh 13:12,15).*

***159. Je, imani ya watu wazima inaweza kufaidisha watoto?***
- Ndiyo, imani ya watu wazima inaweza kufaidisha watoto kama wengine pia. Walimletea Yesu "mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne... Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, 'Mwanangu, umesamehewa dhambi zako" *(Mk 2:5).* Kwa ubatizo watoto wanaunganishwa naye na kuanza kuponywa madonda ya dhambi ya asili. "Tazama, mimi naliumbwa kati hali ya uovu, mama yangu alinichukua mimba hatiani" *(Zab 51:5).* "Ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo" *(Rom 5:19).*

***160. Ubatizo wa watoto wachanga unafanyika tangu lini?***
- Ubatizo wa watoto wachanga unafanyika tangu mwanzo, usipingwe na yeyote kwa miaka elfu na zaidi. Ni kwamba Wayahudi walipokea watoto katika dini yao kwa kuwatahiri siku ya nane baada ya kuzaliwa. "Hata zilipotimia siku nane za kumtahiri, aliitwa jina lake Yesu" *(Lk 2:21).* Watu wa mataifa walipoongokea dini hiyo, walioshwa na kutahiriwa pamoja na watoto wao. Mitume pia walipokea katika Kanisa familia nzima, si wazazi tu. Walibatizwa "yeye na nyumba yake", "yeye na watu wake wote" *(Mdo 16:15,33);* "watu wa nyumbani mwa Stefana" *(1Kor 1:16).*

***161. Je, ubatizo unatosha?***
- Hapana, ubatizo hautoshi, bali unahitaji kukamilishwa na kipaimara na ekaristi, kama vile baada ya kuzaliwa tunahitaji kukomaa na kudumisha uhai wetu kwa chakula. Sakramenti hizo tatu kwa pamoja ni msingi wa maisha ya Wakristo wote, kumbe nyingine zinahitajika tu katika hali na nafasi maalumu. Mitume waliwaendea Wasamaria "wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu" *(Mdo 8:15-16).* "Amin, amin, nawaambieni: Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu" *(Yoh 6:53).*

***162. Sakramenti inayohusiana zaidi na ubatizo ni ipi?***
- Sakramenti inayohusiana zaidi na ubatizo ni kipaimara, kinachoendeleza kazi yake. "Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao" *(Mdo 19:5-6).* Sakramenti hizo ni kama pande mbili za pesa moja. Zinahusiana kama Pasaka na Pentekoste, ambayo ni utimilifu wake, kwa kuwa siku alipofufuka Yesu aliwapulizia Mitume Roho Mtakatifu, ambaye siku hamsini baadaye akawajia kama "upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote" *(Mdo 2:2).*

***163. Pamoja na kuwekewa mikono na mwandamizi wa Mitume, mtu anapewa kipaimara vipi?***
- Pamoja na kuwekea mikono na mwandamizi wa Mitume, mtu anapewa kipaimara kwa kupakwa krisma kama mhuri wa kuwa mali ya Bwana. Ndiyo inayotufanya tuitwe Wakristo nyuma ya Yesu aliyeitwa Kristo. "Kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu" *(Yoh 6:27).* "Yeye atufanyaye imara pamoja nanyi katika Kristo, na kututia mafuta, ni Mungu, naye ndiye aliyetutia muhuri akatupa arabuni ya Roho mioyoni mwetu" *(2Kor 1:21-22).*

***164. Kumpokea Roho Mtakatifu maana yake nini?***
- Kumpokea Roho Mtakatifu maana yake ni kuja kuongozwa naye badala ya kutawaliwa na shetani. "Kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanae mioyoni mwetu, aliaye, 'Aba!' yaani, 'Baba!' Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu. Lakini wakati ule, kwa kuwa hamkumjua Mungu, mliwatumikia wao ambao kwa asili si miungu... Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho" *(Gal 4:6-8; 5:25).* "Ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake" *(Rom 8:9).*

***165. Tukimpokea Roho Mtakatifu papo hapo tunapokea pia nini?***
- Tukimpokea Roho Mtakatifu papo hapo tunapokea pia adili kuu la upendo: "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na

Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" *(Rom 5:5).* Tena tunapokea vipaji vyake ambavyo Yesu alikuwa navyo kikamilifu. "Roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana. Na furaha yake itakuwa katika kumcha Bwana" *(Isa 11:2-3).* Mambo hayo, tofauti na karama, ni ya lazima kwa yeyote apate wokovu wa milele.

***166. Je, tunaweza kuhakikisha neema ya utakaso?***

- Hapana, hatuwezi kuhakikisha neema ya utakaso kwa kuwa ni tukio ambalo linapita maumbile na kufanyika rohoni, hivyo halifikiwi na hisi zetu. Pengine Mungu anatokeza dalili fulani za badiliko hilo kama vile furaha ya ndani au karama ya nje, lakini hizo hazihitajiki wala hazitoshi kuthibitishia mtu amepata neema hiyo. "Wengi wataniambia siku ile: Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri: Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu" *(Math 7:22-23).* "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu" *(1Kor 13:1-3).*

***167. Je, karama ni zile za kushangaza tu?***

- Hapana, karama si zile za kushangaza tu, tena zile muhimu zaidi si hizo, bali zile zinazojenga zaidi Kanisa, kama zile za uongozi: "Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha" *(1Kor 12:28).* "Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; ikiwa huduma, tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha, katika kufundisha kwake; mwenye kuonya, katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimamia, kwa bidii; mwenye kurehemu, kwa furaha" *(Rom 12:6-8).*

***168. Karama nyingine muhimu zinatuwezesha kufanya nini?***

- Karama nyingine muhimu zinatuwezesha kuishi kwa useja kama Yesu na Paulo, au kwa ndoa: "Nipendalo ni kwamba watu wote wawe kama mimi nilivyo; walakini kila mtu ana karama yake mwenyewe itokayo kwa Mungu, huyu hivi, na huyu hivi. Lakini nawaambia wale wasiooa bado, na wajane; ni heri wakae kama mimi nilivyo" *(1Kor 7:7-8).* "Si wote wawezao kulipokea neno hili, ila wale waliojaliwa" *(Math 19:11).* Tunavyoona katika historia ya watawa, mara nyingi karama ya useja inaendana na nyingine katika maisha ya sala, ya kijumuia na ya kitume. Hivyo Filipo "alikuwa na binti wanne, mabikira, waliokuwa wakitabiri" *(Mdo 21:9).*

***169. Karama zinagawiwa vipi?***
- Karama zinagawiwa na Roho Mtakatifu jinsi anavyotaka, si kwa sifa au faida ya binafsi, bali kwa ustawi wa taifa la Mungu. "Kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye... Je, wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri?... Kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenye karama za roho, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa... Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani" *(1Kor 12:11,29-30; 14:12,33).* Kwa ajili hiyo mitume walipambanua na kuratibu karama katika ibada na katika maisha ya jumuia zisije zikavuruga Kanisa.

***170. Karama za kushangaza zina hatari gani?***
- Karama za kushangaza zina hatari mbalimbali, hasa zikitiwa maanani mno. Hapo ni rahisi zilete majivuno, kijicho na mafarakano. "Ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je, si watu wa tabia ya mwili ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?... Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi. Naam, laiti mngemiliki... Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke" *(1Kor 3:3; 4:8; 10:12).* Katika mambo yasiyothibitika ni rahisi kudanganyika kuwa yametoka kwa Mungu, kumbe sivyo. Kisha kudanganyika ni vigumu kuachana nayo hata yakiwa na madhara kwa mhusika au kwa Kanisa. "Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani" *(1Yoh 4:1).*

***171. Tunda la kuongozwa na Roho Mtakatifu ni lipi?***
- Tunda la kuongozwa na Roho Mtakatifu ni umoja wa Kanisa unaotokana na ustawi wa upendo na vipaji ndani ya waamini. "Wote walijaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri. Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja" *(Mdo 4:31-32).* "Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" *(Gal 5:22-23).* "Lakini, mkiwa na wivu wenye uchungu na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani. Maana hapo palipo wivu na ugomvi, ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi; tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki" *(Yak 3:14-17).* Madhehebu yanapozidi kufarakana ni lazima tujiulize kama kweli ni kazi ya Roho Mtakatifu.

***172. Sakramenti inayokamilisha ubatizo na kipaimara ni ipi?***
- Sakramenti inayokamilisha ubatizo na kipaimara ni ekaristi, iliyo kuu kuliko sakramenti zote kwa sababu ndiyo Yesu mzima, Mungu-mtu, katika maumbo ya mkate na divai. Sisi ambao tulishiriki kifumbo kifo na ufufuko

wake tukapokea kwake paji la Roho Mtakatifu, tunaalikwa kukaribia mara kwa mara meza anapotulisha na kutunywesha Mwili na Damu yake ili tushiriki uhai wake kwa dhati zaidi na zaidi. "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake. Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi" *(Yoh 6:56-57).* Ubatizo na kipaimara havirudiwi, vinadumu ndani mwetu kama mifupa ambayo ekaristi ya mara kwa mara inazidi kuitia mwili na damu.

***173. Ekaristi maana yake nini?***
- Ekaristi maana yake ni shukrani, iliyokuwa msimamo wa msingi wa Yesu kwa Baba maisha yake yote, hasa alipofikia wakati wa kutolewa awe kafara ya wokovu wetu. "Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, 'Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu'. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, 'Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu'" *(1Kor 11:23-25).*

***174.Yesu alitumia mkate na divai kwa sababu gani?***
- Yesu alitumia mkate na divai kwa sababu vilikuwa vya maana sana katika utamaduni wake na katika Agano la Kale. Vilikuwa chakula cha kawaida na kinywaji cha karamu. "Divai imfurahishe mtu moyo wake... na mkate umburudishe mtu moyo wake" *(Zab 104:15).* Vilitokana na chembe za ngano na matunda ya mzabibu ambavyo Yesu alijifananisha navyo. "Amin, amin, nawaambia: Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi" *(Yoh 12:24).* "Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi; akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote" *(Yoh 15:5).* Baada ya kulimwa, vilihitaji kusagwa au kushinikizwa, matendo yanayodokeza tena mateso yake pamoja na kazi ya binadamu. Pia wingi wa chembe na wa zabibu zinazoungana ziwe mkate na divai unamaanisha umoja wa waamini ndani ya Kristo. Kwa hiyo ni lazima tutumie daima mkate na divai, si vitu vingine.

***175. Mara nyingi waamini wanapokea umbo la mkate tu kwa lengo gani?***
- Mara nyingi waamini wanapokea umbo la mkate tu kwa lengo la kukwepa umwagaji wa Damu ya Kristo na kurahisisha ibada, hasa kama washiriki ni umati (hata milioni 4 katika misa moja). Yesu mwenyewe alizungumzia mkate kuliko divai, kwa sababu chakula ni muhimu kuliko kileo. "Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka mbinguni; mtu akila chakula hiki, ataishi milele. Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu" *(Yoh 6:51).* "Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" *(1Kor 10:17).* Anayekula umbo la mkate hapokei sehemu tu ya Yesu, bali anampokea mzima, Mwili, Damu,

Roho na Umungu. Pamoja na hayo, daima ni lazima walau padri anywe umbo la divai.

***176. Je, divai ni halali?***

- Ndiyo, divai ni halali, mradi itumike kwa kiasi isije ikaleta madhara. "Melkizedeki mfalme wa Salemu alileta mkate na divai, naye alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu sana" *(Mwa 14:18),* "amefananishwa na Mwana wa Mungu" *(Eb 3:7).* "Bwana wa majeshi atawafanyia mataifa yote karamu ya vitu vinono, karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake, karamu ya vinono vilivyojaa mafuta, karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake, iliyochujwa sana" *(Isa 25:6).* "Njoo, ule mkate wangu, ukanywe divai niliyoichanganya" *(Mith 9:5-6).* Yesu alishiriki karamu nyingi na katika mojawapo ndipo alipoanza miujiza yake kwa kugeuza mapipa ya maji kuwa divai bora. "Kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa" *(Yoh 2:10).* Tujihadhari na hoja za kibinadamu zinazoelekea kumlaumu kwa ajili hiyo, kama wengine walivyofanya zamani zake: "Mwana wa Adamu amekuja, anakula na kunywa, nanyi mwasema, 'Tazama, mlafi huyu, na mnywaji wa divai, rafiki wao watoza ushuru na wenye dhambi" *(Lk 7:34).*

***177. Hatimaye Yesu alitumia divai kufanyia nini?***

- Hatimaye Yesu alitumia divai kutuachia ishara ya damu yake tuweze kushiriki mateso yake. "Je, mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi?" *(Math 20:22).* Kisha kushiriki kila mwaka karamu ya Pasaka, ambapo wote walikunywa divai mara nne, safari ya mwisho alikamilisha miujiza yake kwa kuigeuza iwe damu yake. "'Nimetamani sana kuila Pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu'. Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, 'Twaeni hiki, mgawanywe ninyi kwa ninyi; maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja'. Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, 'Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu'. Kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kula, akisema, 'Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu'" *(Lk 22:15-20).* "Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je, si ushirika wa damu ya Kristo?" *(1Kor 10:16).*

***178. Katika karamu ya Bwana tunakula na kunywa nini?***

- Katika karamu ya Bwana tunakula na kunywa Mwili wa Damu ya Kristo. Katika sala kuu ya ekaristi padri anaporudia maneno ya Yesu juu ya mkate na divai, Roho Mtakatifu anavigeuza kwa dhati: mkate si tena mkate, wala divai si tena divai, ingawa maumbo yanabaki yaleyale kwa hisi zetu. "Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli" *(Yoh 6:54-55).*

"Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana" *(1Kor 11:27).*

***179. Baada ya mageuzo Yesu anabaki katika ekaristi mpaka lini?***

- Baada ya mageuzo Yesu anabaki katika ekaristi moja kwa moja. Maumbo ya mkate na divai yanazidi kudokeza uwepo wake kama chakula na kinywaji chetu, hata kwa faida ya wagonjwa na wengineo wasiohudhuria. Ndiyo sababu tunazidi kumuabudu katika ekaristi, ingawa hatumuoni. "Tomaso alijibu, akamwambia, 'Bwana wangu na Mungu wangu!' Yesu akamwambia, 'Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki" *(Yoh 20:28-29).*

***180. Je, ekaristi ni kafara?***

- Ndiyo, ekaristi ni kafara ambayo Yesu alimtolea Baba msalabani na anaendelea kumtolea kwa wokovu wetu. "Yeye, kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee... Kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe vipawa na dhabihu; kwa hiyo lazima huyu naye awe na kitu cha kutoa" *(Eb 7:24-25; 8:3).* Katika ekaristi tunajiunga naye kwa kufanya ukumbusho wa kifo na ufufuko wake, tukimtolea tena Baba sadaka ya Mwili na Damu yake iliyolinganishwa na zile za Waisraeli na za Wapagani: "Waangalieni hao Waisraeli walivyokuwa kwa jinsi ya mwili; wale wazilao dhabihu, je, hawana shirika na madhabahu? Basi niseme nini? Ya kwamba kile kilichotolewa sadaka kwa sanamu ni kitu? Au ya kwamba sanamu ni kitu? Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo sadaka wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. Hamwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani" *(1Kor 10:18-21).*

***181. Kwa nini ekaristi inaitwa sakramenti ya upendo?***

- Ekaristi inaitwa sakramenti ya upendo kwa sababu kila tunapofanya ukumbusho wa sadaka hiyo pekee tunazidi kujifunza na kupokea upendo ambao siku hiyo Yesu "ali amewapenda watu wake katika ulimwengu, aliwapenda upeo" *(Yoh 13:1).* Hivyo tunawezeshwa kutekeleza amri mpya aliyotuachia pamoja na ekaristi. "Amri mpya nawapa: Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo" *(Yoh 13:34).* Ni sharti tujitoe kama Yesu, tukijiunga na sadaka yake katika ibada na katika maisha. "Katika hili tumelifahamu pendo: kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu. Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma yake, je, upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo? Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli" *(1Yoh 3:16-18).*

***182. Ekaristi inaadhimishwa kwa mpangilio gani?***

- Ekaristi inaadhimishwa kwa mpangilio wa kupanda: tunalishwa Neno la Mungu katika mimbari, halafu Mwili na Damu ya Kristo katika altare. Vilevile sehemu ya kwanza (liturujia ya Neno) inatuletea masomo yakiwa na kilele katika Injili. Halafu katika sehemu ya pili (liturujia ya ekaristi) padri anafuata alichofanya Yesu katika karamu ya mwisho: anatwaa mkate na divai (kuandaa dhabihu zetu), anashukuru juu yake (sala kuu ya ekaristi inayogeuza dhabihu) na kuwapa waamini (komunyo, kilele cha yote, inayotugeuza ndani ya Kristo). Yesu mfufuka "aliwaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe... Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua" *(Lk 24:27,30-31).* "Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali" *(Mdo 2:42).* "Siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu... akamega mkate, akala" *(Mdo 20:7,11).* Tusipofuata vizuri hatua za awali, hatutafaidika kweli na sakramenti: ndiyo sababu ni muhimu tuwahi ibada.

## SAKRAMENTI ZA UPONYAJI

***183. Yesu aliweka Kitubio na Mpako wa Wagonjwa kwa sababu gani?***

- Yesu aliweka Kitubio na Mpako wa Wagonjwa kwa sababu alijua udhaifu wa binadamu hauishi mara anapopokea uzima wa Mungu kwa sakramenti tatu za kuingizwa katika Ukristo. Hivyo alipanga kusaidia mpaka mwisho wa dunia waamini wake watakaopatwa na dhambi na ugonjwa, kama alivyowasaidia wengi aliokutana nao katika maisha yake. "Yesu, alipoiona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza, 'Jipe moyo mkuu, mwanangu, umesamehewa dhambi zako'... 'Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi' – amwambia yule mwenye kupooza – 'Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako'. Akaondoka, akaenda zake nyumbani kwake. Makutano walipomwona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii" *(Math 9:2,6-8).*

***184. Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi kwa njia ya nani?***

- Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi kwa njia ya Mwanae. Yesu mfufuka aliwaonyesha Mitume alama ya mateso mwilini mwake, "akawavuvia, akawaambia, 'Pokeeni Roho Mtakatifu. Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wowote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa" *(Yoh 20:22-23).* Katika Kanisa tunafurahi kupewa msamaha wa dhambi kila tunapohitaji, mradi tutubu. Kwa njia ya

mwandamizi wa Mitume, Yesu anatuambia, "Umesamehewa dhambi zako... Imani yako imekuokoa, enenda zako kwa amani" *(Lk 7:48,50).* Si dhana wala hisia tu, bali ni neno la hakika tunalolipokea kwa masikio yetu.

***185. Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi zipi?***
- Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi zote, kwa sababu upendo mtiifu wa Mwanae aliyejitoa kuwa sadaka ya wokovu wetu unampendeza kuliko dhambi zote zinavyomchukiza. Ila hatuwezi kusamehewa dhambi ya kukataa neema ambayo Roho Mtakatifu anatusukuma tuamini na kutubu, kwa sababu pasipo imani na toba hapana msamaha. "Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa" *(Math 12:31).* "Nasi tukitenda kazi pamoja naye twawasihi msiipokee neema ya Mungu bure" *(2Kor 6:1).*

***186. Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi kwa sababu gani?***
- Mungu aliwapa watu amri ya kusamehe dhambi kwa sababu amependa washiriki katika kazi zake. Ametuumba kwa njia ya wazazi na kutulea na kutusaidia kwa njia ya wengine pia. Hasa ametuokoa kwa njia ya Yesu, ambaye yupo nasi sikuzote katika Mwili wake, yaani Kanisa, na katika wale walioshirikishwa mamlaka ya Mitume. "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo: mpatanishwe na Mungu" *(2Kor 5:18-20).*

***187. Je, tumuendee padri ili kuondolewa dhambi?***
- Ndiyo, tumuendee padri ili kuondolewa dhambi tulizotenda baada ya ubatizo, kwa kuwa hatuwezi kupokea msamaha tukikataa masharti yake, na Mungu ametupangia watu ambao watuondolee kwa niaba yake. "Watu wote na watoza ushuru waliposikia hayo, waliikiri haki ya Mungu, kwa kuwa wamebatizwa kwa ubatizo wa Yohane. Lakini, Mafarisayo na wanasheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye" *(Lk 7:29-30).* Yesu mwenyewe alikubali kubatizwa na Yohane ili atimize mpango wa Baba. "Yohane alitaka kumzuia, akisema, 'Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?' Yesu akajibu akamwambia, 'Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote" *(Math 3:14-15).* Je, sisi tukatae kumkimbilia padri wa Mungu ili kupokea huruma yake tunayoihitaji kuliko hewa?

***188. Tumuungamie padri dhambi zetu kwa lengo gani?***
- Tumuungamie padri dhambi zetu ili aweze kutushauri na kuamua kama tuko tayari kuondolewa. Tumweleze kwa unyofu makosa yote tuliyoyafanya na nia tuliyonayo ya kuyafidia na kutoyarudia. "Tukisema

kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo, wala neno lake halimo mwetu" *(1Yoh 1:8-10).* Tukumbuke tulivyo viungo vya Mwili mmoja, hivi kwamba dhambi zetu zimewadhuru wenzetu. "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana, mpate kuponywa" *(Yak 5:16).* Kutokuwa tayari kufanya hivyo walau sirini kwa padri ni dalili ya kiburi na ya kutotubu.

***189. Je, padri akiwa mkosefu, anaweza kutuondolea dhambi?***

- Ndiyo, padri akiwa mkosefu, anaweza kutuondolea dhambi kwa niaba ya Mungu aliyempa mamlaka hiyo. Hatusamehewi na utakatifu wa padri, bali na huruma ya Baba kwa njia yake. Yeye anamtumia padri yeyote ili kuturahisishia kazi, tusihitaji kuchunguza kwanza ubora wa maisha yake, wala kwenda mbali tukampate mmoja asiye na dhambi. Tungefanyeje kuhakikisha ni mtakatifu, wakati hatuwezi kusoma moyo wake? Ingekuwa hivi, tusingepata kamwe hakika ya kusamehewa. Kumbe inatutosha kujua ni padri, kwamba Mungu amempa mamlaka ya kusamehe dhambi, kama Yesu alivyowapa Mitume siku tatu baada ya kumkimbia na hata kumkana. Kila padri anaweza kukiri, "Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa: ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi, ambao wa kwanza wao ni mimi" *(1Tim 1:15).* Amri ya kusamehe dhambi wamepewa watu, si malaika. "Tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu" *(2Kor 4:7).*

***190. Je, nje ya kitubio tunaweza kuondolewa dhambi tuliyotenda baada ya ubatizo?***

- Ndiyo, nje ya kitubio tunaweza kuondolewa dhambi tuliyotenda baada ya ubatizo, lakini ni vigumu zaidi, kwa sababu hatupati msaada wa sakramenti hiyo maalumu. Pamoja na nia ya kumuungamia padri mapema tunahitaji neema ya kutubu kikamilifu, si kwa kuhofia adhabu, bali kwa kumpenda Mungu tuliyemchukiza. "Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana" *(Lk 7:47).*

***191. Mpako wa Wagonjwa ulianzishwa na nani?***

- Mpako wa Wagonjwa ulianzishwa na Yesu, kama sakramenti zote. Maandiko yanasimulia huruma yake iliyomfanya awaponye wengi kwa namna mbalimbali na kuwapa Mitume uwezo wa kufanya vilevile kwa "kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina" *(Math 10:1).* Nao "wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawapoza" *(Mk 6:13).* "Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa, nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa" *(Yak 5:14-15).*

***192. Mafuta ya wagonjwa yanamaanisha nini?***
- Mafuta ya wagonjwa yanamaanisha lengo la kuwaponya na kuwarudishia nguvu na uzuri. Kama kawaida, maneno yanaweka wazi zaidi kuwa lengo si kuponya mwili tu, bali hasa roho kwa kuitia msamaha na faraja katika mateso ambayo huenda yakaendelea. Kwa kuwa Mungu haponyi mwili kila mara, isipokuwa kwa faida na wokovu wa mgonjwa na wa wengine. Kama ndiyo mapenzi yake, kila mmoja ajifunze kufaidika vilevile na ugonjwa: "Makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, 'Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu'. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu" *(2Kor 12:7-9).* "Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake" *(Kol 1:24).*

## SAKRAMENTI ZA KUHUDUMIA USHIRIKA NA UTUME

***193. Daraja na ndoa ni tofauti na sakramenti nyingine kwa sababu gani?***
- Daraja na ndoa ni tofauti na sakramenti nyingine kwa sababu hazilengi hasa faida ya mtu anayezipokea, bali huduma zake kwa ajili ya Kanisa na jamii. Daraja inatia uwezo wa Kristo kwa ustawi wa Kanisa, Bibi arusi wake. Ndoa inatia upendo wake mwaminifu kwa ustawi wa familia, kanisa dogo la nyumbani. "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe" *(Mdo 20:28).* "Hakuna mtu anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa" *(Ef 5:29-32).*

***194. Je, daraja takatifu zinahitajiwa kabisa na Kanisa?***
- Ndiyo, daraja takatifu zinahitajiwa kabisa na Kanisa kwa sababu kazi ya wokovu haimtegemei binadamu, bali Mungu. "Hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni. Vivyo hivyo Kristo naye hakujitukuza nafsi yake kufanywa kuhani mkuu" *(Eb 5:4-5),* bali alisisitiza alivyopewa na Baba uwezo wa kutuokoa. "Baba ampenda Mwana, naye amempa vyote mkononi mwake" *(Yoh 3:35).* "Kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote

uliompa awape uzima wa milele” *(Yoh 17:2).* Kisha kufufuka alitumia mamlaka hiyo kuwatuma wanafunzi kumi na mmoja waliobaki: “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari” *(Math 28:18-20).* Mpaka mwisho wa dunia uwezo huo wa Kimungu utatolewa tu kwa sakramenti ya daraja, inayounganisha mtu na Mitume kupitia mlolongo usiokatika wa kuwekewa mikono ili kushirikishwa mamlaka. Bila yake, kuna upungufu katika ufundishaji, utoaji wa sakramenti na uongozi.

***195. Je, wenye daraja wanastahili heshima?***

- Ndiyo, wenye daraja wanastahili heshima kwa sababu ya mamlaka ya Kiroho waliyonayo kutoka kwa Kristo. “Amin, amin, nawaambieni: Yeye ampokeaye mtu yeyote nimpelekaye, anipokea mimi; naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenipeleka” *(Yoh 13:20).* “Jaribu lililowapata katika mwili wangu hamkulidharau wala kulikataa, bali mlinipokea kama malaika wa Mungu, kama Kristo Yesu” *(Gal 4:14).* “Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii” *(Tito 3:1).* Wenye daraja wanaotimiza kazi zao vizuri wanastahili heshima kwa uaminifu wao pia. “Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu, hasa hao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha” *(1Tim 5:17).*

***196. Je, wenye daraja wanaweza wakatenda dhambi?***

- Ndiyo, wenye daraja wanaweza wakatenda dhambi kwa sababu ni binadamu kama sisi sote. Yesu alionja ukosefu wa Mitume hasa wakati wa mateso. “Je, mimi sikuwachagua ninyi Thenashara, na mmoja wenu ni shetani?” *(Yoh 6:70).* “Tazama, saa yaja, naam, imekwisha kuja, ambapo mtatawanyika kila mmoja kwao, na kuniacha mimi peke yangu” *(Yoh 16:32).* Paulo alionya mapadri, “Katika ninyi wenyewe watainuka watu, wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao” *(Mdo 20:30).*

***197. Ili tuwe na wachungaji wengi waaminifu tunapaswa kufanya nini?***

- Ili tuwe na wachungaji wengi waaminifu tunapaswa hasa kusali. “Mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake” *(Math 9:38).* Halafu yanahitajika maandalizi ya muda mrefu, juhudi na ushirikiano wa kidugu. “Asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi... Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia... Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine” *(1Tim 3:6; 4:16; 5:22).*

***198. Je, wanawake wanaweza kupewa daraja?***

- Hapana, wanawake hawawezi kupewa daraja, kwa sababu kwa karibu

miaka elfu mbili mfululizo Kanisa limejiona halina mamlaka ya kufanya tofauti na Yesu. Yeye alichagua wanaume tu kuwa Mitume wake, ingawa walikuwepo wanawake waaminifu kuliko wengi wao, hasa Maria, mtakatifu kuliko wote. "Petro, na Yohane, na Yakobo, na Andrea, Filipo na Tomaso, Bartholomayo na Mathayo, Yakobo wa Alfayo, na Simoni Zelote, na Yuda wa Yakobo. Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake... Wakaweka wawili, Yusufu, aitwaye Barsaba, aliyekuwa na jina la pili Yusto, na Mathiya... kura ikamwangukia Mathiya; naye akahesabiwa kuwa pamoja na mitume kumi na mmoja" *(Mdo 1:13-14,23,26).* "Walimchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, na Prokoro, na Nikanori, na Timoni, na Parmena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia; ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba wakaweka mikono yao juu yao" *(Mdo 6:5-6).*

***199. Je, kutoa daraja kwa wanaume tu ni kuwakosea haki wanawake?***
- Hapana, kutoa daraja kwa wanaume tu si kuwakosea haki wanawake, kwa kuwa hizo ni huduma zinazofaidisha wote. "Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani, au yule atumikaye? Siye yule aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye" *(Lk 22:27).* Mwenye daraja anahudumia Kanisa kwa kumwakilisha Yesu; hivyo anatakiwa kuwa mwanamume kama yeye mbele ya Bibiarusi wake. Kukubali mgawanyo wa majukumu maishani ni kusifu hekima ya Mungu aliyetuumba watu wa jinsia mbili tofauti ili kustawisha familia, jamii na Kanisa. "Walakini si mwanamke pasipo mwanamume, wala mwanamume pasipo mwanamke, katika Bwana... Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake" *(1Kor 11:11; 12:27).*

***200. Je, mwenye daraja anaweza kuwa na ndoa?***
- Ndiyo, mwenye daraja anaweza kuwa na ndoa. "Hatuna uwezo kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa?" *(1Kor 9:5).* Paulo, akiwa mseja, hakudai kila mmojawao aoe, ila asiwe ameoa mara mbili, bali "mume wa mke mmoja" *(1Tim 3:2; Tit 1:6),* kama alivyoagiza mjane aandikishwe akiwa tu "mke wa mume mmoja" *(1Tim 5:9).* Polepole mang'amuzi yakaelekeza Kanisa kubana nafasi hiyo kwa Maaskofu, na katika majimbo mengi kwa mapadri pia. Useja mtakatifu unawalinganisha zaidi na Yesu na kuwaachia uhuru wa moyo na wa muda kwa ajili ya huduma. "Wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee" *(Math 19:12).*

***201. Kadiri ya mpango wa Muumba, ndoa halisi ina sifa ngapi?***
- Kadiri ya mpango wa Muumba, ndoa halisi ina sifa tatu: umoja, uimara na utayari wa kuzaa. "Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, 'Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe, na hao

wawili watakuwa mwili mmoja?’ Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe” *(Math 19:4-6).* “Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, ‘Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha’” *(Mwa 1:28).* Mitara, uzinifu, talaka, ushoga na kukataa uzazi ni kinyume cha mpango huo.

***202. Yesu aliweka sakramenti ya ndoa kwa sababu gani?***
- Yesu aliweka sakramenti ya ndoa kwa sababu ya umuhimu wa familia kwa ustawi wa mume na mke, watoto, jamii na ufalme wa Mungu, na kwa sababu ya uzito wa majukumu yanayohusika. “Siku ya tatu palikuwa na arusi huko Kana, mji wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwepo. Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake” *(Yoh 2:1-2),* akaleta divai bora ya ndoa sakramenti badala ya ndoa ya kimaumbile. Hivyo ametuandalia neema tuweze kushinda “ugumu wa mioyo” *(Math 19:8)* unaohatarisha daima uzuri wa mpango wa Mungu kuhusu upendo mwaminifu katika ndoa. “Mungu aliona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana” *(Mwa 1:31).*

***203. Ndoa ya Wakristo ni sakramenti ya nani?***
- Ndoa ya Wakristo ni sakramenti ya Yesu na Kanisa lake. “Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi arusi, mke wa Mwanakondoo” *(Ufu 21:9).* Wakiwa na ndoa halisi, mume na mke waliobatizwa ni ishara wazi ya hao wanaarusi wawili wasioonekana. “Kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake” *(Ef 5:24-25).* Ndiyo sababu Mkatoliki hawezi kufunga ndoa bila ya kuhusisha Kanisa na kufuata taratibu zake.

## IBADA NYINGINE

***204. Mbali ya sakramenti, Kanisa linamuadhimisha Mungu vipi?***
- Mbali ya sakramenti, Kanisa linamuadhimisha Mungu hasa kwa Liturujia ya Vipindi, yaani kwa sala rasmi zinazotolewa mara kadhaa kwa siku, kufuatana na ratiba ya binadamu ya usiku na mchana. Hivyo linajitahidi kutimiza agizo la kusali daima. “Imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa” *(Lk 18:1).* “Kesheni ninyi kila wakati, mkiomba” *(Lk 21:36).* “Ombeni bila kukoma, shukuruni kwa kila jambo” *(1Thes 5:17).* “Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote” *(Ef 6:18).* “Huyo amemwekea Mungu tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku” *(1Tim 5:5).*

***205. Kanisa linamuadhimishaje Mungu tena?***

- Kanisa linamuadhimisha Mungu tena kwa visakramenti ambavyo kwa mamlaka ya Kristo linawatia watu neema zake katika nafasi yoyote ya maisha. Kati yake muhimu zaidi ni baraka na mazinguo, ambavyo vipo tangu zamani, hata nje ya taifa la Israeli. Melkisedek alisema, "Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi. Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako" *(Mwa 14:19-20).* Farao aliomba, "Mkanibariki mimi pia" *(Kut 12:32).* Balaam alisifiwa, "Najua ya kuwa yeye umbarikiye hubarikiwa, na yeye umlaaniye hulaaniwa" *(Hes 22:6).* "Ikawa, ile roho mbaya kutoka kwa Mungu ilipomjilia Sauli, ndipo Daudi akakishika kinubi, akakipiga kwa mkono wake, naye Sauli akaburudishwa, na ile roho mbaya ikamwacha" *(1Sam 16:23).* "Na mimi nikitoa pepo kwa Beelzebuli, je, wana wenu huwatoa kwa nani?" *(Math 12:27).*

***206. Maana ya baraka ni ipi?***
- Maana ya baraka ni kumsifu Mungu kwa yale aliyokwishatujalia na kumuomba azidi kutujalia kadiri ya mahitaji ya wahusika. Mara nyingi inatolewa na mtu mwenye daraja au mamlaka fulani. Yesu aliletewa "watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea" *(Math 19:13).* Siku ya kupaa mbinguni "aliinua mikono yake akawabariki" *(Lk 24:50).* "Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao" *(Mdo 13:3).* Pengine vinabarikiwa vitu vinavyotumiwa na watu, au mahali wanapoishi. "Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni akavibariki, akavimega, akawapa wanafunzi wake ili wawaandikie mkutano" *(Lk 9:16).*

***207. Mazinguo ndiyo nini?***
- Mazinguo ni sala za kupungia mashetani ili kuepusha watu na balaa au madhara, hasa kama wamepagawa nao. "Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu" *(Mk 5:8).* "Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena!" *(Mk 9:25).* Yesu ameliachia Kanisa mamlaka yake juu yao. "Aliwaita wale Thenashara, akaanza kuwatuma wawili wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu" *(Mk 6:7).* "Paulo alisikitika, akageuka akamwambia yule pepo, 'Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu'. Akamtoka saa ileile" *(Mdo 16:18).*

***208. Kanisa linatoa visakramenti kwa nani?***
- Kanisa linatoa visakramenti hata kwa waamini wenye vizuio na kwa wasio Wakristo, kwa sababu vinaeleweka na kuthaminiwa kwa urahisi, kwa kuwa zinasaidia kufurahia maisha. "Ikawa katika njia kuu hutoa nje wagonjwa, na kuwaweka juu ya majamvi na magodoro, ili Petro akija, ngawa kivuli chake kimwangukie mmojawapo wao. Nayo makutano ya watu wa miji iliyoko kandokando ya Yerusalemu wakakutanika, wakileta wagonjwa, nao walioudhiwa na pepo wachafu; nao wote wakaponywa" *(Mdo 5:15-16).* "Mungu alifanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida; hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao yakawaondokea, pepo wachafu wakawatoka" *(Mdo*

*19:11-12).*

***209. Lengo kuu la visakramenti ni lipi?***
- Lengo kuu la visakramenti ni kuwaandaa watu wapokee kwa imani sakramenti zitakazowatia uzima wa Mungu unaodumu milele. Hivyo visakramenti visitiwe maanani kuliko sakramenti zilizowekwa na Yesu mwenyewe ziwe kiini cha maisha yetu. "Amin, amin, nawaambieni: Ninyi mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba. Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele, ambacho Mwana wa Adamu atawapa" *(Yoh 6:26-27).* Sakramenti zinatujaza baraka na kutukinga kuliko kisakramenti chochote.

***210. Kanisa linaheshimu marehemu kwa namna gani?***
- Kanisa linaheshimu marehemu kwa kuwafanyia mazishi huku likiwaombea kwa Mungu. "Watu watauwa walimzika Stefano, wakamfanyia maombolezo makuu" *(Mdo 8:2).* Yeye kama mfiadini, aliyefikia upeo wa upendo kwa kutoa uhai wake, hakuhitaji kuombewa. Lakini wafu wengine walitolewa sala na sadaka tangu Israeli ilipoanza kusadiki ufufuo. "Kama asingalitumaini kuwa wale waliokufa watafufuka, ingalikuwa kazi bure isiyo na maana kuwaombea wafu. Lakini kwa kuwa aliufikiri utukufu wa thawabu waliowekewa wale wafao katika utauwa, wazo lake lilikuwa takatifu na la kicho. Ndiyo sababu alifanya upatanisho kwa wafu ili wafunguliwe dhambi yao" *(2Mak 12:44-46).* "Kama wafu hawafufuliwi kamwe, kwa nini kubatizwa kwa ajili yao?" *(1Kor 15:29).*

***211. Je, ni halali kwa Wakristo kujitungia ibada nyingine?***
- Ndiyo, ni halali kwa Wakristo kujitungia ibada nyingine, mradi wakubali zipimwe na Maaskofu kama zinalingana na imani, maadili na taratibu za Kanisa. "Mtu asiwanyang'anye thawabu yenu, kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe tu, na kuabudu malaika, akijitia katika maono yake na kujivuna bure... Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu" *(Kol 2:18,23).* "Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao" *(2Tim 3:14).*

***212. Ni halali kujitungia ibada kwa sababu gani?***
- Ni halali kujitungia ibada kwa sababu sala ni hasa maongezi ya Mungu na mtu. Adamu na Eva "walisikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga" *(Mwa 3:8).* Yeye hachoki kumvuta kila mmojawetu kwake na kumtia hamu ya kumhimidi na kumuabudu, kumuomba kwa ajili yake na ya wengine, kumshukuru na kumsifu. "Ee Bwana, uisikie sala yangu, uzisikilize dua zangu, kwa uaminifu wako unijibu kwa haki yako" *(Zab 143:1).* Hata tukisali pamoja, uhusiano wa kila mmojawetu na Mungu ni wa pekee. Tusiposali kwa moyo, ibada ni ya

bure. “Watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana nami” *(Isa 29:13).*

***213. Ikiwa sala ni maongezi ya Mungu na mtu, kwanza tufanye nini?***

- Ikiwa sala ni maongezi ya Mungu na mtu, kwanza tumsikilize kwa makini na kutafakari alichosema ili tukifanyie kazi. Tukisema peke yetu si sala, kwa kuwa ukisema upande mmoja tu si maongezi. “Nena, Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikia” *(1Sam 3:10).* “Nakutafakari Wewe makesha yote ya usiku” *(Zab 63:6).* “Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa” *(Zab 119:97).* “Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu” *(Yer 15:16).*

***214. Kielelezo cha sala yetu ni nani?***

- Kielelezo cha sala yetu ni Yesu Kristo. “Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, ‘Bwana, tufundishe sisi kusali” *(Lk 11:1).* Yeye kama binadamu alichota humo uaminifu kwa wito wake wa pekee. “Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe” *(Yoh 17:1).* “Aba, Baba, yote yawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe” *(Mk 14:36).*

***215. Kama binadamu Yesu alijifunza kusali kwa nani?***

- Kama binadamu Yesu alijifunza kusali kwa Mama yake na kwa mapokeo yote ya Israeli, yaliyojitokeza hasa katika Zaburi. “Wazee wake huenda Yerusalemu kila mwaka, wakati wa sikukuu ya Pasaka. Na alipopata umri wake miaka kumi na miwili, walipanda kama ilivyokuwa desturi ya sikukuu” *(Lk 2:41-42).* “Saa tisa Yesu alipaza sauti yake kwa nguvu, ‘Eloi, Eloi, lama sabakthani?’” *(Mk 15:34).* “Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu” *(Lk 23:46).*

***216. Je, sala ya Yesu inatokana na utu wake tu?***

- Hapana, sala ya Yesu haitokani na utu wake tu, bali katika huo Mwana wa milele ndiye anayemuelekezea Baba yake sala kamili ya kitoto. “Saa ileile alishangilia kwa Roho Mtakatifu, akasema, ‘Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha wenye hekima na akili, umewafunulia watoto wachanga. Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyokupendeza” *(Lk 10:21).* “Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia sikuzote” *(Yoh 11:41-42).* “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo” *(Lk 23:34).*

***217. Yesu alisali vipi?***

- Yesu alisali kila mahali na kila wakati, akidumisha ushirika wa upendo kati yake na Baba katika Roho Mtakatifu. “Saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu” *(Yoh 4:23).* Pamoja

na kushiriki kiaminifu ibada za taifa lake, mara nyingi alijitafutia mahali pa faragha. "Aliongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani" *(Lk 4:1).* "Alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba" *(Lk 5:16).* "Aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu" *(Lk 6:12).* Ndiyo sababu ametuambia, "Wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini" *(Math 6:6).* Tusipojua kuongea na Baba moyo kwa moyo, tutawezaje kuongea naye kati ya umati?

***218. Yesu ametufundisha kusali vipi?***
- Yesu ametufundisha kusali akitueleza misimamo ambayo tuwe nayo. "Upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako... Waombeeni wanaowaudhi... Msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu" *(Math 5:24,44; 6:5).* "Mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipigapiga kifua akisema, 'Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi'. Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki" *(Lk 18:13-14).* Hasa ametutia Roho Mtakatifu atuongoze kama alivyomfanyia yeye.

***219. Je, Yesu ametufundisha maneno ya sala pia?***
- Ndiyo, Yesu ametufundisha maneno ya sala ya 'Baba Yetu', kamili kuliko zote. Maombi yake saba yanategemea utangulizi ambao tunamuendea Mungu kwa ujasiri na furaha kama watoto wake, ndugu kati yetu. Maombi matatu ya kwanza yanalenga atukuzwe, atawale, apate ushirikiano wetu. Maombi manne ya mwisho yanalenga tupate chakula cha roho na cha mwili, msamaha wa dhambi, ushindi katika vishawishi, usalama dhidi ya yule Mwovu. "Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba. Basi ninyi salini hivi..." *(Math 6:8-9).*

***220. Je, sala inategemea maneno?***
- Hapana, sala haitegemei maneno mengi mazuri, bali kujijenga "juu ya imani... na kuomba katika Roho Mtakatifu" *(Yud 20).* "Mkiwa katika kusali, msipayukepayuke, kama watu wa mataifa; maana hao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi" *(Math 6:7).* Hii haituzuii tusirudie maneno yetu kwa dhati zaidi na zaidi. Yesu "alikwenda, akaomba mara ya tatu, akisema maneno yaleyale" *(Math 26:44).* Tunaweza kusali kimoyomoyo pia. "Hana alikuwa akinena moyoni mwake, midomo yake tu ilionekana kama anena, sauti yake isisikiwe... 'Nimeimimina roho yangu mbele za Bwana'" *(1Sam 1:13,15).* "Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana" *(Zab 19:14).*

***221. Je, sala yetu inasikilizwa daima?***
- Ndiyo, sala yetu inasikilizwa daima kwa kuwa imeunganika kwa imani na

ile ya Yesu, njia pekee ya kumuendea Baba. "Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata, furaha yenu iwe timilifu" *(Yoh 16:24).* Lakini Baba, kwa ujuzi na upendo usio na mipaka, anaweza akatupatia mambo tofauti na yale tuliyomuomba. "Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, 'Nipe maji ninywe', ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai" *(Yoh 4:10).* "Ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" *(Lk 11:13).* Imani yetu ikubali kwamba aliyotupatia ni bora zaidi.

***222. Je, sala inaweza kumuendea Yesu?***
- Ndiyo, sala inaweza kumuendea Yesu, Bwana wetu na kaka yetu, aliye hai mbinguni, kama ilivyomuendea na kusikilizwa alipokuwa duniani. Mhalifu alisema, "'Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako'. Yesu akamwambia, 'Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi" *(Lk 23:42-43).* Stefano aliomba, "'Bwana Yesu, pokea roho yangu'. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, 'Bwana, usiwahesabie dhambi hii'" *(Mdo 7:59-60).* "Roho na Bibi arusi wasema, 'Njoo!'. Naye asikiaye na aseme, 'Njoo!'... Na uje, Bwana Yesu!" *(Ufu 22:17,20).*

***223. Roho Mtakatifu anatusaidiaje kusali?***
- Roho Mtakatifu anatusaidia tusali kama Yesu, akiwa mlezi wa ndani na kutumia vipaji vyake saba. "Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, 'Aba!' yaani, 'Baba!'" *(Gal 4:6)*. "Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa... huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu" *(Rom 8:26-27).* Ndiyo sababu Kanisa linatuhimiza tumtamani na kumualika kila mara, 'Njoo, Roho Mtakatifu!' yaani kumuomba Baba kwa njia ya Mwana amtume zaidi na zaidi ndani mwetu.

***224. Roho Mtakatifu anaweza kutufikisha hadi wapi ?***
- Roho Mtakatifu anaweza kutufikisha hadi muungano wa dhati na Mungu. Yeye "awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu" *(Ef 3:16-19).* "Huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote" *(Yoh 16:13).* Safari hiyo inategemea sana sala isiyoishia katika maneno bali inalenga kupenya mafumbo kwa imani na upendo.

***225. Je, sala inaweza kuwaendea Mama na marafiki wa Yesu?***
- Ndiyo, sala inaweza kuwaendea Mama na marafiki wa Yesu, walioungana naye kuwa mwili mmoja, wasiweze kutenganishwa na chochote. "Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima,

wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine chochote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu” *(Rom 8:38-39).* “Kwangu mimi kuishi na Kristo, na kufa ni faida... Ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo” *(Fil 1:21,23).* Kwa kuwa hao wako na Kristo mbinguni, wanatuombea mfululizo pamoja naye. “Niliona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, ‘Ee Mwenyezi, Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini...’” *(Ufu 6:9-10).* Tunawaomba wazidi kutuombea kwa Mungu, kama tunavyowaomba wenzetu waliopo duniani. “Mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote; pia na kwa ajili yangu mimi” *(Ef 6:18-19).*

## MUHTASARI: SALA YA BWANA

Ndugu, tukariri maneno ya sala
ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake.
Ndiyo muhtasari wa Injili yake yote.
Ndiyo kiini cha ibada zote za Kanisa.
Ndiyo sala ya watoto wa Mungu
tunayokabidhiwa katika ubatizo
ili tustawishe siku kwa siku
chini ya Roho Mtakatifu
fungamano letu na Baba.

**Baba yetu uliye mbinguni,**
**jina lako litukuzwe,**
**ufalme wako ufike,**
**utakalo lifanyike duniani kama mbinguni.**
**Utupe leo mkate wetu wa kila siku.**
**Utusamehe makosa yetu kama tunavyowasamehe na sisi waliotukosea.**
**Usitutie katika vishawishi,**
**lakini utuopoe maovuni.**
**Amina.**